JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA UJENZI


Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
S. L. P 2888,
**40470 DODOMA.**


**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na. EA. 163/194/01

17 Julai, 2025


ENGINEERS REGISTRATION BOARD
RECEIVED
22 JUl 2025
DODOMA


**Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS),
S. L. P 11364,
**DODOMA**.

**Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Majengo Tanzania (TBA),
Mtaa wa Uhindini Dodoma,
S. L. P 902,
**DODOMA.**

**Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA),
Jengo la TEMESA,
NCC – Mtaa wa Tambukareli,
S. L. P 1075,
**DODOMA.**

**Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mfuko,**
Bodi ya Mfuko wa Barabara,
Jengo la Mfuko wa Barabara,
Eneo la Uwekezaji la Njedengwa,
Kiwanja Na.03 Kitalu D,
S. L. P 993,
**DODOMA**.

**Msajili,**
Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo
na Wakadiriaji Majenzi (AQRB),
Makao Makuu Dodoma,
9 Mtaa wa *AQRB*,
S. L. P 2377,
41101 Tambukareli,
**DODOMA.**

**Msajili**,
Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB),
3 Barabara ya Ukaguzi,
S. L. P 2768,
**41104 DODOMA.**

**Msajili**,
Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB),
Mkandarasi Place,
S. L. P 96,
**DODOMA.**

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC),
RFB Building,
Ground Floor
Block D-Plot Na. 3, Njedengwa
S. L. P 1236,
**DODOMA**.

**Mkuu wa Taasisi,**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT),
S. L. P 963,
**MOROGORO.**

**Mkuu wa Vikosi vya Ujenzi**,
S. L. P 879,
**DODOMA.**

**Yah: KATAZO LA KUTUMA BARUA, TAARIFA NA NYARAKA ZA SERIKALI KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII NA BARUA PEPE ZISIZOKUWA ZA KISERIKALI**

Tafadhali rejeeni somo lililotajwa hapo juu.

2. Kama mnavyofahamu, Utumishi wa Umma unaongozwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuhakikisha Wananchi wanapata huduma bora kwa urahisi na haraka zaidi.

3. Hivi karibuni kumekuwepo na baadhi ya Watumishi wa Umma ambao wamekuwa wanatumiana barua, taarifa na nyaraka mbalimbali za kiofisi kupitia mitandao ya kijamii na barua pepe zisizokuwa za Serikali (GMS) kinyume cha Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma.

4. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 (Sura ya 273) Kifungu cha 57 na 58 ni makosa kwa Mtumishi wa Umma kushirikisha (share), kufichua, kutuma au kusambaza kutoka Ofisi ya Umma, kwa mtu au makundi sogozi *(Whatsapp Group)* kupitia mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp, Instagram, Facebook* au barua pepe isiyokuwa ya Serikali kama vile *yahoo mail, gmail, Hotmail* n.k.

5. Kwa mujibu wa mwongozo wa matumizi bora, sahihi na salama wa vifaa, Data na mifumo ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2022 kipengele cha 3.3 njia iliyoidhinishwa ya usambazaji wa taarifa, barua na nyaraka ni kupitia mfumo wa barua pepe za Serikali (GMS). Hivyo kutuma nyaraka, barua na madokezo kupitia barua pepe zisizokuwa za Serikali au mitandao ya kijamii ni kosa kwa mujibu wa Sheria.

6. Mtumishi wa Umma atakayepatikana na hatia kwa kosa la kushirikisha *(share),* kufichua, kutuma au kusambaza barua, Dokezo, Taarifa au Nyaraka ya Serikali kupitia mitandao ya kijamii au barua pepe zisizo za Serikali adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano (5,000,000/=) na isiyozidi shilingi milioni kumi (10,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote kwa pamoja.

7. Aidha, Mtumishi atakayetiwa hatiani kutokana na makosa hayo kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, Kanuni ya 42 (1) adhabu yake ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo au kupunguzwa mshahara.

8. Kwa barua hii, tafadhali zingatieni Taratibu na Miongozo hii na waelekezeni Watumishi walio chini yenu kuacha mara moja kushirikisha, kutuma au kusambaza nyaraka mbalimbali za Ofisi kupitia mitandao ya kijamii na barua pepe zisizokuwa za Serikali (GMS).

9. Mtumishi yoyote ayakayebainika kukaidi maelekezo haya atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kupelekwa katika vyombo vya kisheria.

10. Ninawatakia utekelezaji mwema.

M. S. Mrisho
**Kny. KATIBU MKUU**